ISSN 0856 - 0331X

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

# *ACT SUPPLEMENT*

*No. 23* *18th September, 2015*

*to the Gazette of the United Republic of Tanzania No. 38 Vol. 96 dated 18th September, 2015*
Printed by the Government Printer, Dar es Salaam by Order of Government

## THE TANZANIA EXTRACTIVE INDUSTRIES (TRANSPARENCY AND ACCOUNTABILITY) ACT, 2015

### ARRANGEMENT OF SECTIONS

*Section* *Title*

PART I
PRELIMINARY PROVISIONS

1. Short title and commencement.
2. Application.
3. Interpretation.

PART II
ADMINISTRATIVE PROVISIONS

4. Establishment of Committee.
5. Composition of the Committee.
6. Nomination Committee.
7. Functions of the Nomination Committee.
8. Tenure of office.
9. Proceedings of the Committee.
10. Functions and powers of the Committee.
11. Delegation of powers.
12. Appointment of Executive Secretary.
13. Secretariat.

PART III
OBLIGATION OF EXTRACTIVE COMPANIES AND STATUTORY RECIPIENTS

14. Threshold and obligation of extractive companies and statutory recipients.
15. Information on local content, corporate social responsibility and capital expenditures.
16. Obligation to publish information.

# SHERIA YA UWAZI NA UWAJIBIKAJI KATIKA RASILIMALI ZA MADINI, MAFUTA NA GESI ASILIA TANZANIA, 2015

## MPANGILIO WA VIFUNGU

*Kifungu* *Jina*

### SEHEMU Y A KWANZA
### MASHARTI YA UTANGULIZI

1. Jina la Sheria na tarehe itakapoanza kutumika.
2. Matumizi
3. Tafsiri

### SEHEMU YA PILI
### MASHARTI YA UTAWALA

4. Kuanzishwa kwa Kamati ya TEITI.
5. Muundo wa Kamati.
6. Kamati ya Uteuzi.
7. Majukumu ya Kamati ya Uteuzi.
8. Muda wa kuwa madarakani
9. Taratibu za Kamati.
10. Kazi na mamlaka ya Kamati.
11. Kukasimu Madaraka.
12. Uteuzi wa Katibu Mtendaji.
13. Sekretarieti.

SEHEMU YA TATU
WAJIBU WA MAKAMPUNI NA TAASISI ZA SERIKALI ZINAZOKUSANYA MAPATO KUTOKA TASNIA UZINDUAJI

14. Wajibu wa Makampuni na Taasisi za Serikali zinazokusanya mapato kutoka Tasnia Uziduaji
15. Taarifa kuhusu malipo kwa bidhaa na huduma zinazopatikana nchini, gharama za uwekezaji na katika miradi ya jamii.
16. Wajibu wa kutoa Taarifa.

SEHEMU YA NNE
UTEUZI NA MAJUKUMU YA MLINGANISHI WA MALIPO NA MAPATO

17. Uteuzi na majukumu ya mlinganishi wa malipo na mapato

SEHEMU YA TANO
JUKUMU LA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI NA TOFAUTI ZA MALIPO NA MAPATO

18. Jukumu la Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali na tofauti za malipo na mapato

SEHEMU YA SITA
MASHARTI YA JUMLA

19. Waziri kuwasilisha Taarifa
20. Vyanzo vya mapato ya Kamati.
21. Mahesabu na Ukaguzi.
22. Taarifa ya mahesabu ya mwaka.
23. Makosa na adhabu.
24. Taarifa za uongo.
25. Mamlaka ya kutengeneza Kanuni
26. Mamlaka ya Waziri kutangaza rasilimali za tasnia ya uiduaji
27. Kifungu cha hifadhi.

SEHEMU YA SABA
MABADILIKO YATOKANAYO

28. Construction.
29. Amendment of section 4.
30. Amendment of section 6.
31. Amendment of section 7.
32. Amendment of section 11.
33. Amendment of section 21.
34. Amendment of section 22.
35. Addition of new section 22A.
36. Amendment of section 25.
37. Amendment of section 26.
38. Amendment of section 28.
39. Amendment of section 32.
40. Amendment of section 39.
41. Amendment of section 40.
42. Amendment of section 41.
43. Amendment of section 47.
44. Amendment of section 52.
45. Amendment of section 54.
46. Amendment of section 55.
47. Amendment of section 58.
48. Amendment of section 65.
49. Amendment of section 73.
50. Amendment of section 77.
51. Amendment of section 79.
52. Amendment of section 86.
53. Amendment of section 90.
54. Amendment of section 95.

*(d) Amendment of the Electricity Act*
*(Cap. 131)*

55. Construction.
56. Amendment of section 41.

*(e) Amendment of the Income Tax Act,*
*(Cap.332)*

57. Construction.
58. Amendment of section 140.

## JEDWALI

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

NA.23 YA 2015

NAKUBALI,

JAKAYA MRISHO KIKWETE,

*Rais*

4 Agosti, 2015

**Sheria ya Uwazi na Uwajibikaji Katika Rasilimali za Madini, Mafuta na Gesi Asilia Tanzania kwa ajili ya kuboresha Usimamizi, uwajibikaji na kuanzishwa kwa Kamati ya kusimamia utekelezaji wa Sheria hii.**

**IMETUNGWA** na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

SEHEMU YA KWANZA
VIFUNGU VYA UTANGULIZI

Jina la Sheria na tarehe itakapoanza kutumika.

**1.** Sheria hii itaitwa Sheria ya Uwazi na Uwajibikaji katika Rasilimali za Madini, Mafuta na Gesi Asilia Tanzania, 2015 na itaanza kutumika katika tarehe ambayo Waziri anaweza, kwa taarifa itakayochapishwa kwenye *Gazeti* la Serikali, kuiteua.

Matumizi

**2.** Sheria hii itatumika Tanzania Bara.

Tafsiri

**3.** Katika Sheria hii isipokuwa kama muktadha utahitaji vinginevyo:

"Kamati" ni Kamati ya Uwazi na Uwajibikaji katika Tasinia ya Uziduaji Tanzania. iliyoanzishwa chini ya kifungu cha 4;

Sura ya 418

"Mkaguzi na Mdhibiti ·Mkuu wa Hesabu za Serikali" ni Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali aliyeanzishwa na Sheria ya Ukaguzi wa Umma;

"Mwenyekiti" ni Mwenyekiti wa Kamati aliyeteuliwa chini ya kifungu cha 5.;

"Katibu Mtendaji" ni Katibu Mtendaji aliyeteuliwa chini ya kifungu cha 12;

"tasnia ya uziduaji" kwa madhumuni ya Sheria hii, maana yake ni tasnia inayohusisha maliasili za madini, mafuta na gesi asilia na maliasili nyingine;

"kampuni za uziduaji" maana yake ni kampuni zinazojishughulisha na utafutaji na uchimbaji wa maliasili za madini, gesi asilia na mafuta;

"uwazi katika tasnia ya uziduaji" pia inayojukana kama "EITI" maana yake ni viwango vya Kimataifa vya uwazi na uwajibikaji katika tasnia ya uziduaji vinavyosimamiwa;

"mlinganishi huru wa malipo na mapato" ni mtaalamu mshauri aliyesajiliwa kisheria kwa kazi ya ukaguzi wa mahesabu chini ya kifungu cha 14;

"ushirikishwaji wa watanzania" maana yake ni juhudi za kuongeza ushiriki wa watanzania katika utoaji wa huduma, bidhaa, teknolojia, ajira na utaalamu kwenye uendeshaji wa tasnia ya uziduaji;

"Waziri" maana yake ni Waziri anayehusika na masuala yanayohusu madini, mafuta na gesi asilia;

"Taasisi za Serikali" maana yake ni Taasisi za Serikali zinazohusika katika kukusanya mapato yanayotokana na tasnia ya uziduaji;

"kamati ndogo" maana yake ni kmati ndogo inayoundwa chini ya aya ya 14 ya Jedwali la sheria hii..

## SEHEMU YA PILI
## MASHARTI YA UTAWALA

Kuanzishwa kwa Kamati ya TEITI

**4.**-(1) Itaanzishwa Kamati itakayojulikana kama Kamati ya TEITI itakayosimamia Mpango wa Uwazi na Uwajibikaji katika Tasnia ya Uziduaji Tanzania.

(2) Kamati itakuwa ni chombo huru cha Serikali cha kusimamia utekelezaji wa shughuli za uimarishaji uwazi na uwajibikaji katika tasnia ya uziduaji.

Muundo wa Kamati

**5.**-(1) Kamati itaundwa na Mwenyekiti atakayeteuliwa na Rais wa Jamhuri wa Muungano wa Tanzania na wajumbe wengine wasiopungua kumi na tano wenye uelewa na ujuzi katika masuala ya tasnia ya uziduaji.

(2) Wajumbe wengine kumi na tano ni kama ifuatavyo:

(a) wajumbe watano watakaoteuliwa na Waziri kutoka Taasisi za Serikali zinazohusika katika kukusanya mapato yanayotokana na Kampuni za Uziduaji akiwemo Mwanasheria Mkuu wa Serikali au Mwakilishi wake;

(b) wajumbe watano kutoka kampuni za uziduaji ; na

(c) wajumbe watano kutoka asasi za kiraia zinazojihusisha na shughuli za tasnia ya uziduaji.

(3) Katibu Mtendaji ambaye atakuwa katibu wa Kamati.

(4) Wajumbe waliotajwa chini ya kifungu kidogo cha (1) (b) na (c) watateuliwa na Taasisi zao kufuatana na taratibu walizojiwekea.

Kamati ya Uteuzi

**6.**-(1) Kutakuwa na Kamati itakayojulikana kama Kamati ya Uteuzi.

(2) Kamati ya Uteuzi itaundwa na wajumbe wafuatao-

(a) Katibu Mkuu wa Wizara inayohusika masuala ya madini ambaye atakuwa Mwenyekiti wa Kamati ya Uteuzi;

(b) Katibu Mkuu wa Wizara inayohusika na masuala ya fedha;

(c) Katibu Mkuu wa Wizara inayohusika na masuala ya utumishi wa umma;

(d) Katibu Mkuu wa Wizara inayohusika na masuala ya kazi; na

(e) wataalam wawili katika masuala ya uziduaji.

(3) Mmoja kati ya wajumbe wawili wanaorejewa katika kifungu kidogo cha (2)(e) atateuliwa na Waziri kutoka miongoni mwa majina matatu yatakayowasilishwa na makampuni ya uziduaji na mtu mwingine atatoka miongoni mwa majina matatu yaliyowasilishwa na umoja wa asasi za kiraia.

(4) Kamati ya Uteuzi haitakuwa ya kudumu itatekeleza majukumu yake pale uteuzi utakapohitajika.

(5) Kamati italipa posho, ada na gharama nyingine zitakazotumikia na Kamati ya Uteuzi kama zitakavyoidhinishwa na Waziri.

Majukumu ya kamati ya uteuzi

7.-(1) Kamati ya Uteuzi itaitisha maombi, itachambua na kupendekeza majina ya watu kwa ajili ya uteuzi katika nafasi ya-

(a) Mwenyekiti wa Kamati ya Uwazi na Uwajibikaji katika Tasnia ya Uziduaji Tanzania; na

(b) Katibu Mtendaji wa Kamati;

(2) Kamati ya Uteuzi inaweza kuchukua hatua muhimu kutambua na kuwavutia waombaji wanaofaa kupitia matangazo. yatakayotolewa kwenye magazeti yanayosomwa maeneo mengi nchini.

(3) Kamati ya Uteuzi itawasilisha kwa Waziri-

(a) kwa nafasi ya Mwenyekiti, majina matatu yatakayopelekwa na Waziri kwa Rais kwa ajili ya uteuzi wa Mwenyekiti; na

(b) kwa nafasi ya Katibu Mtendaji, majina matatu kwa ajili ya uteuzi wa Katibu Mtendaji.

(4) Kamati ya uteuzi itasimamia mwenendo wa majadiliano na masuala mengine yanayohusu Kamati hiyo.

Muda wa kuwa madarakani

**8.** Mwenyekiti na wajumbe wa Kamati watakaa madarakani kwa kipindi cha miaka mitatu na wanaweza kuteuliwa kwa kipindi kingine kimoja cha miaka mitatu.

Taratibu za kamati

**9.** Masharti ya jedwal la sheria hii yatafafanua uendeshaji wa mikutano ya Kamati.

Kazi na Mamlaka ya Kamati

**10.**-(1) Kamati itakuwa na jukumu la kuhakikisha kuwa mapato ya tasnia ya uziduaji yanahakikiwa na kutumika kwa manufaa ya wananchi wote.

(2) Kwa kuzingatia kifungu cha (1) Mamlaka ya Kamati na kazi zake ni kama ifuatavyo-

(a) Kuandaa mfumo wa uwekaji uwazi wa taarifa za malipo kutoka kampuni za uziduaji na mapato yaliyopokelewa Serikalini;

(b) Kuzitaka kampuni zote za uziduaji na taasisi za Serikali kutoa taarifa sahihi juu ya malipo na mapato yaliyokusanywa na taasisi hizo katika mwaka wa fedha husika;

(c) kuzitaka kampuni za uziduaji kuwasilisha kwenye Kamati gharama za uwekezaji, takwimu za uzalishaji na mauzo ya nje katika kila mwaka wa fedha;

(d) kuhamasisha ufahamu juu ya mchango wa tasnia ya uziduaji na maendeleo yake kiuchumi na kijamii pamoja na kuhamasisha ushiriki wa wananchi katika tasnia ya uziduaji;

(e) kufanya uchunguzi wa tofauti za hesabu zilizojitokeza katika ulinganishi wa malipo na mapato yanayotokana na tasnia ya uziduaji kulingana na vifungu vya Sheria hii;

(f) kufanya ulinganishi wa hesabu za malipo na mapato yaliyokusanywa na taasisi za serikali kutoka makampuni ya uziduaji;

(g) kubaini tofauti na kuchukua hatua zinazofaa katika kuimarisha taasisi za Serikali au halmashauri zenye mamlaka ya kukusanya mapato kutoka kampuni za uziduaji;

(h) kusambaza kwa njia ya machapisho taarifa za ulinganishi na uchunguzi au taarifa yeyote inayohusu mapato yaliyopokelewa na taasisi za Serikali kutoka kampuni za uziduaji; na

(i) kusimamia majukumu ya Sekretarieti;

(j) kufanya tafiti au mafunzo kwa lengo la kuendeleza majukumu ya Kamati; na

(k) kutekeleza majukumu mengine kwa lengo la kuwezesha shughuli za Kamati.

(3) Kamati itawasilisha kwa Waziri Ripoti ya utekelezaji wa shughuli zote zilizotajwa katika kifungu kidogo cha (2) kwa ajili ya hatua stahiki katika kuboresha usimamizi wa tasnia ya uziduaji.

Kukasimu madaraka

**11.** Kamati inaweza kukasimu madaraka yake kwa Kamati ndogo itakayoziunda au kwa Sekretarieti.

Katibu Mtendaji

**12.**-(1) Atakuwepo Katibu Mtendaji wa Kamati atakayeteuliwa na Waziri.

(2) Katibu Mtendaji atakuwa Katibu wa Kamati na atakuwa Afisa masuhuli wa Sekretarieti na atatekeleza shughuli za kila siku za Kamati.

(3) Mtu atateuliwa kuwa Katibu Mtendaji iwapo mtu huyo atakuwa na sifa zifuatazo-

(a) awe na angalau shahada katika taaluma ya uhandisi, uchumi, sheria, stadi za maendeleo, jiolojia na fedha.

(b) uzoefu katika maswala ya tasnia ya uziduaji kwa muda usiopungua miaka tano.

(4) Katibu Mtendaji atateuliwa kwa kipindi cha miaka mitano na anaweza kuteuliwa kwa kipindi kingine kimoja.

Sekretarieti

**13.**-(1) kutakuwepo na Sekretarieti ya Kamati itakayokuwa na jukumu la kutekeleza shughuli za kila siku za Kamati.

(2) Maafisa na wafanyakazi wa Sekretarieti watakuwa watumishi wa Umma.

## SEHEMU YA TATU
## WAJIBU WA MAKAMPUNI NA TAASISI ZA SERIKALI ZINAZO-KUSANYA MAPATO KUTOKA TASNIA YA UZIDUAJI

Wajibu wa Makampuni na Taasisi za Serikali zinazokusanya mapato kutoka Tasnia Uziduaji

**14.**-(1) Kamati itaweka kiwango cha chini cha malipo ya kodi kila mwaka wa fedha kwa ajili ya kuainisha kampuni zitakazotakiwa kuwasilisha taarifa za malipo kwa ajili ya kazi ya ulinganishi wa malipo hayo na mapato yaliyopokelewa na taasisi za Serikali.

(2) Kampuni ya uziduaji ambayo malipo yake ya kodi yatazidi kiwango kilichowekwa katika kifungu kidogo cha (1) itatakiwa kuwasilisha taarifa na takwimu za malipo katika utaratibu utakaowekwa katika kanuni, kwa aina zote za malipo ya kodi yaliyofanywa Serikalini.

(3) Taasisi za Serikali zinazokusanya malipo kutoka kampuni za uziduaji zitawasilisha kwenye Kamati taarifa na takwimu za mapato yaliyopokelewa kutoka kampuni za uziduaji.

Taarifa kuhusu Malipo kwa Bidhaa na Huduma kutoka ndani ya nchi, gharama za uwekezaji na katika Miradi ya Jamii

**15.**-(1) Kampuni zilizopo kwenye tasnia ya uziduaji zitawasilisha katika kila mwaka wa fedha taarifa za malipo kwa bidhaa na huduma kutoka ndani ya nchi, gharama za uwekezaji na katika miradi ya Jamii.

(2) Bila kujali kifungu kidogo cha (1), kampuni za uziduaji zitawasilisha kwenye Kamati gharama zilizotumika katika kila hatua ya uwekezaji.

(3) Mtu yeyote au kampuni itakayoshindwa kuwasilisha taarifa zinazotajwa katika kifungu hiki atakuwa ametenda kosa.

Wajibu wa Kutoa Taarifa

**16.** Katika kuhakikisha uwazi na uwajibikaji katika tasnia ya uziduaji, Kamati itamuwezesha Waziri kuweka wazi-

(a) Mikataba na Leseni za kampuni za uziduaji katika tovuti au kutumia Chombo cha Habari kilicho na uwezo wa kuwafika wananchi wengi nchini;

(b) majina ya wamiliki wa hisa na wenye maslahi katika kampuni za uziduaji;
(c) ripoti za utekelezaji wa mipango ya utunzaji wa mazingira unaofanywa na kampuni za uziduaji chini ya kifungu cha 17.

## SEHEMU YA NNE
## UTEUZI NA MAJUKUMU YA MLINGANISHI WA MALIPO NA MAPATO

Uteuzi na Majukumu ya Mlinganishi wa malipo na mapato

**17.**-(1) Kamati itaajiri mlinganishi huru wa taarifa za malipo yanayofanywa na kampuni za uziduaji na mapato yanayokusanywa na Taasisi za Serikali.

(2) Taarifa ya ulinganishi itajumuisha taarifa na takwimu za gharama za uwekezaji, uzalishaji, mauzo ya nje na shughuli zozote zinazoendana na tasnia ya uziduaji kwa kila mwaka wa fedha.

(3) Mlinganishi wa taarifa aliyeteuliwa na Kamati anapaswa kuwa mwenye sifa na uzoefu wa kufanya kazi za ulinganishi kama inavyoneshwa katika kifungu kidogo cha (1) na (2).

(4) Mlinganishi wa malipo na mapato atafanya kazi ya ulinganishi kulingana na hadidu za Rejea kama zilivyowekwa na Kamati.

(5) Mlinganishi atawasilisha taarifa baada ya zoezi la ulinganisho kwenye Kamati kwa ajili ya kupitiwa na kupata ridhaa kabla ya kuchapishwa na kutolewa kwa umma.

## SEHEMU YA TANO
## JUKUMU LA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI NA TOFAUTI ZA MALIPO NA MAPATO

Jukumu la Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali na tofauti za malipo na mapato cap. 418

**18.**-(1) Endapo ripoti ya ulinganishi wa malipo na mapato yanayotokana na tasnia ya uziduaji itaonesha tofauti kati malipo na mapato inayozidi asilimia moja ya mapato yote yaliyoripotiwa kupokelewa Serikalini, Kamati inatakiwa ndani ya siku kumi na nne, kuwasilisha

ripoti hiyo kwa Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa uchunguzi.

(2) Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali anapaswa kuandaa ripoti ya uchunguzi na kuiwasilisha kwenye Kamati na kwa Waziri kwa mapitio na taarifa.

(3) Kamati inatakiwa baada ya kuwasilishwa kwa ripoti ya uchunguzi kama inavyotajwa kwenye kifungu kidogo cha (2) kuiwasilisha taarifa hiyo kwenye mamlaka husika kwa hatua zaidi.

(4) Mamlaka husika baada ya kupokea ripoti ya uchunguzi kutoka kwenye Kamati inatakiwa kuchukua hatua za utekelezaji wa mapendekezo yaliyomo kwenye ripoti hiyo ndani ya siku thelathini na kurejesha taarifa ya utekelezaji kwenye Kamati.

(5) Kamati inatakiwa ndani ya siku kumi na nne baada ya kupokea taarifa ya utekelezaji kama iliyotajwa katika kifungu kidogo cha (4) kuiwasilisha kwa Waziri kwa mapitio na kuchapisha kwenye tovuti na vyombo vya Habari.

## SEHEMU YA SITA
## MASHARTI YA JUMLA

Waziri kuwasilisha Taarifa

**19.** Waziri anapaswa kwa wakati unaofaa na sio zaidi ya miezi kumi na mbili baada kufungwa kwa mwaka wa fedha, kuwasilisha kwenye Bunge taarifa za utekelezaji wa shughuli za Kamati zilizoainishwa chini ya Sheria hii.

Vyanzo vya mapato

**20.** Vyanzo vya mapato vitajumuisha-

(a) kiasi cha fedha ambazo zitaidhinishwa na Bunge;

(b) kiasi chochote cha fedha ambacho kimekopwa na Kamati kutoka ndani au nje ya Tanzania;

(c) kiasi chochote cha fedha au mali ambacho Kamati inaweza kulipwa au kuwekezwa kwenye Kamati chini ya Sherai hii au sheria nyingine yoyote kulingana na suala lolote katika utekelezaji wa majukumu yake.

**Mahesabu na ukaguzi**

**21.**-(1) Kamati itahifadhi kumbkumbu sahihi za ukaguzi kuhusiana na-

(a) kiasi cha fedha kilichopokelewa na kutumika;

(b) vitega uchumi vya Kamati;

(c) taarifa ya mapato na matumizi ya Kamati.

(2) Ukaguzi wa fedha utafanywa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali au mtu mwingine yeyopte aliyeidhinishwa naye.

**Taarifa ya mahesabu ya mwaka**

**22.**-(1) Kabla ya miezi sita katika mwaka wa fedha, Kamati itaandaa taarifa ya ukaguzi wa shughuli za kamati na kuiwasilisha kwa Waziri

(2) Miezi sita baada ya taarifa ya ukaguzi, Waziri ataiwasilisha taarifa hiyo Bungeni.

**Makosa na adhabu**

**23.** Mtu yeyote, ambaye bila sababu ya msingi, atashindwa kuwasilisha nyaraka au taarifa zinazotajwa chini ya Sheria hii ndani ya muda uliotajwa, atakuwa ametenda kosa na akihukumiwa adhabu ni kama ifuatavyo-

(a) endapo ni wa mtu binafsi atatozwa faini isiyopungua shilingi million kumi; na

(b) endapo ni Kampuni, atatozwa faini isiyopungua shilingi millioni mia moja na hamsini.

**Taarifa za Uongo**

**24.**-(1) Mtu yeyote ambaye-

(a) atawasilisha taarifa za uongo juu ya ghrama za uwekezaji, uzalishaji, mauzo ya nje na shughuli zozote zinazoendana katika tasnia ya uziduaji au ;

(b) atakayetoa taarifa za uongo juu ya akaunti kushindwa kuwasilisha akaunti chini ya Sheria hii,

bila sababu yeyote ya msingi kukwamisha au kuweka kikwazo kwa Kamati katika kutekeleza majukumu yake, atakuwa ametenda kosa na akihukumiwa atatozwa faini isiyozidi shilingi millioni mia moja.

Mamlaka ya kutengeneza Kanuni

**25.** Waziri kwa kushauriana na Kamati, atatengeneza Kanuni itakayooanisha masuala ya uratibu katika kuwezesha utekelezaji wa vifungu vilivyopo kwenye Sheria hii.

Mamlaka ya kutangaza rasilimali za tasnia ya uziduaji

**26.** Waziri kupitia *Gazeti* la Serikali atatoa tamko na kutangaza rasilimali nyingine kuwa chini ya utekelezaji wa sheria hii.

Kifungu cha hifadhi

**27.**-(1) Mikataba yote ya Madini, Gesi asilia na Mafuta iliyotiliwa sahihi kabla ya Sheria hii, itakapoanza kutumika sheria hii, mikataba hiyo itawekwa wazi kwa kuzingatia matakwa ya uwekaji wazi wa mikataba chini ya Sheria hii.

(2) Isipokuwa kwa taarifa ambazo ni muhimu kutowekwa wazi kwa mujibu wa Waziri atakavyoona inafaa, taarifa nyingine zozote zilizomo ndani ya mikataba kwa maana ya kifungu kidogo cha (1) itawekwa wazi kulingana na vifungu vya Sheria hii.

## SEHEMU YA SABA
## MABADILIKO YATOKANAYO

*(a) Amendment of the Mining Act,*
*(Cap.123)*

Construction Cap. 123

**28.** This Part shall be read as one with the Mining Act, hereinafter referred to as the "principal Act."

Amendment of section 4

**29.** The principal Act is amended in section 4 by-

(d) deleting the definition of the term "Agency";

(e) deleting the definition of the term "primary mining licence" and substituting for it the following:

"primary mining licence" means a licence for small scale mining characterised by minimal machinery or technology of an